**JIJI LA BURLINGTON**
**IDARA YA KAZI ZA UMMA**
**KITENGO CHA RASILIMALI ZA MAJI**
235 Penny Lane | P O Box 878 | Burlington, VT 05402
**Simu** 802.863.4501 | **Faksi** 802.864.8233
water-resources@burlingtonvt.gov | www.burlingtonvt.gov/water

# Mradi wa Orodha ya Nyenzo Zinazounda Mabomba ya Huduma ya Maji

## MASWALI YANAYOULIZWA SANA

### *Mradi wa Orodha ya Nyenzo Zinazounda Mabomba ya Huduma ya Maji ni nini?*

Jiji la Burlington linashirikiana na Jimbo la Vermont na Shirika la Ulinzi wa Mazingira la Marekani kukidhi sharti la kitaifa la kutambua na kuondoa vyanzo vinavyowezekana vya risasi kutoka kwa maji ya kunywa ya umma. Kama sehemu ya sharti hili, Idara ya Rasilimali za Maji ya Burlington inahitajika kuthibitisha au kutambua nyenzo zilizotumika kuunda kila bomba la huduma ya maji katika Jiji. Jiji halina rekodi yoyote ya mabomba yaliyopo yenye risasi na haitarajii kupata mabomba yoyote yenye risasi; hata hivyo orodha hii ni fursa nzuri kwetu kutambua mabomba ya huduma ya maji na sehemu ambazo zinaweza kuhitaji ubadilishaji ili kudumisha ubora wa maji na shinikizo la maji, kama vile mabomba ya zamani ya maji ya mabati, mita za maji, au viunganisho vingine.

### *Je, kuna risasi kwenye maji yangu ya kunywa?*

Kuna uwezekano mdogo sana wa risasi kuwepo katika maji yako ya kunywa ya Burlington. Risasi inaweza kuingia kwenye maji ya kunywa wakati nyenzo za mabomba zenye risasi zinapopata kutu. Kutu ni uyeyushaji na uchakavu wa chuma unaosababishwa na mmenyuko wa kemikali kati ya maji na mabomba yako. Ili kuzuia kutu, Idara ya Rasilimali za Maji ya Burlington huongeza kemikali inayoitwa Zinc Orthophosphate kwenye maji yanayosambazwa kabla ya kuachiliwa kwenye kituo chetu za kutakasa maji. Zinc Orthophosphate hufunika upande wa ndani wa mabomba na mifereji ya maji ya kunywa, na hivyo kuzuia kutu na kupunguza uwezekano wa risasi kuwa katika maji.

Jiji la Burlington halina rekodi zozote za mabomba yaliyopo ya maji yenye risasi katika Jiji na haitarajii kupata mabomba yoyote yenye risasi, kwani kwa kawaida nyenzo hizi hazikutumika ndani ya Burlington. Nyumba zingine za zamani zilizo na mabomba ya chuma ya mabati bado zinaweza kuwa na kiwango kidogo cha risasi katika mfumo wao kupitia viunganishi vifupi kati ya mabomba na bomba kuu vinavyoitwa 'goosenecks', lakini havizingatiwi kuwa vipengele vyenye athari ya risasi chini ya Marekebisho ya Kanuni ya Risasi na Shaba ya EPA. Aidha, kiasi kidogo cha risasi kinaweza kuwepo katika mabomba ya ndani (kwa mfano, paipu, lehemu, mifereji, vifaa, nk.) ya nyumba za zamani, au katika mita za maji zilizowekwa kabla ya mwaka wa 2001, lakini pia haipaswi kuathiri viwango vya risasi katika maji kutokana na vidhibiti vyetu vyenye ufanisi vya kutakasa maji (yaani, matumizi ya vizuia kutu).

### *Je, kwa nini ushiriki wangu ni muhimu?*

Mradi huu utahakikisha tunafuata kanuni mpya ya EPA ya kutambua mabomba yoyote ya maji yenye risasi na kutambua mabomba ya mabati ambayo kwa kawaida huvuja, kuharibika na kupunguza shinikizo la maji baada ya muda kutokana na uwepo wa mashapo ndani ya bomba.

Kuna zaidi ya mabomba 11,000 ya maji yaliyoundwa kwa nyenzo ambazo zinahitaji kutambuliwa au kuthibitishwa ndani ya chini ya mwaka mmoja. Kutokana na upeo na muda wa sharti hili, tunahitaji wateja wa Idara ya Rasilimali za Maji ya Burlington kushiriki ili kutusaidia kupunguza gharama zetu za shughuli hii. Kupunguza gharama za shughuli hutusaidia kutoa maji kwa bei nafuu, kwa viwango vya ushindani na kuwapa wateja wetu mipango ya ziada za mapunguzo ya bei na malipo.

### *Je, mnakusanya taarifa hizi vipi?*

Mbali na kufanya uchambuzi wa kina wa rekodi za kihistoria na za sasa za ufungaji wa mabomba, kimsingi tunategemea umma kushiriki katika utafiti wetu. Pia tutafanya ziara za nyumbani kwa nyumba zinazohitaji ufuatiliaji na kutembelea mitaa ya zamani (mitaa iliyoanzishwa kabla ya mwaka wa 1938). Kutokana na upeo wa mradi huu, tunakuhimiza sana uchukue hatua kwa kujaza utafiti huu, pamoja na maswali yoyote ya ufuatiliaji ya baadaye ambayo tunaweza kuwa nayo kuhusu nyumba yako.

### *Je, mtafanyia nini taarifa hizi?*

Idara ya Rasilimali za Maji ya Burlington itachapisha hadharani ramani ya matokeo yetu ili wakazi waweze kuangalia taarifa za mfumo wao katika siku zijazo. Ikiwa tutapata mabomba yanayohitaji kubadilishwa, Idara ya Rasilimali za Maji ya Burlington itaanzisha Awamu ya II ya mradi huu ili kushirikiana na wamiliki wa mali kubadilisha mabomba yao ya huduma ya maji.

### *Je, mtakuja kuchimba bustani yangu?*

Hapana, awamu hii ya mradi haihitaji uchimbaji katika mali yoyote. Utaarifiwa ikiwa tumetambua mabomba yako ya maji kuwa yanayohitaji kufanyiwa uchunguzi zaidi wakati wa Awamu ya II ya mradi huu.

### *Je, shughuli hii itanigharimu pesa zozote?*

Kutambua nyenzo zilizounda mabomba yako ni bure, hata ikiwa una hali maalum ambayo inahitaji ziara ya nyumbani kutoka kwa Idara ya Rasilimali za Maji ya Burlington. Ikiwa mabomba yako yana risasi (ingawa kuna uwezekano mdogo), yatabadilishwa bila gharama kwako.

### *Je, Kanuni ya Risasi na Shaba ya EPA ni nini?*

Kanuni ya Risasi na Shaba ya EPA ni kanuni iliyowekwa mwaka wa 1991 ambayo inabainisha viwango vya juu vya shaba na risasi katika mifumo ya usambazaji wa maji na inayokusudiwa kuondoa vyanzo vya risasi kutoka kwa maji yetu ya kunywa. Kanuni hii husasishwa kulingana na sayansi ya hivi karibuni. Sasisho la hivi karibuni, linaloitwa Marekebisho ya Kanuni ya Risasi na Shaba, linahitaji watoa huduma wote wa maji kurekodi nyenzo zilizounda mabomba yote ya maji yaliyo chini ya mteja na idara katika eneo lao la huduma kufikia Oktoba 2024. Ikiwa mabomba yoyote ya mabati yanayohitaji ubadilishaji au mabomba yenye risasi yatatambuliwa, idara ya huduma inahitajika kushirikiana na wateja kuyabadilisha bila gharama kwa mteja.

### *Je, mabomba ya huduma ya maji ni nini?*


Mabomba ya huduma ya maji ni mabomba ambayo hubeba maji kutoka kwa bomba kuu la maji la Jiji la Burlington hadi kwenye mali ya mtu binafsi. Kwa kawaida mali nyingi huwa na bomba moja la huduma, lakini zingine zitakuwa na mabomba tofauti ya huduma ya maji kwa ajili ya ulinzi wa moto, umwagiliaji, au matumizi mengine yasiyo ya kunywa. Aina ya nyenzo zinazounda mabomba yote ya huduma lazima irekodiwe kama sehemu ya mradi huu.

### *Je, Vyuma vya Mabati Vinavyohitaji Ubadilishaji (Galvanized Requiring Replacement, GRR) ni nini?*

Vyuma vya Mabati Vinavyohitaji Ubadilishaji vinarejelea mabomba ya maji yaliyoundwa kwa chuma cha mabati yaliyo au ambayo yalikuwa katika upande wa "chini" wa bomba la maji lenye risasi, au kwa sasa yako upande wa chini wa bomba ambalo hali yake ya risasi haijulikani.

### *Je, nitapataje bomba langu la huduma ya maji?*

Bomba la huduma ya maji huingia kwenye mali kupitia msingi wa sehemu ya chini ya nyumba au ukuta (kwa kawaida katika upande wa barabara) na huunganisha na mita ya maji. Ikiwa mali yako haina sehemu ya chini ya nyumba basi angalia katika eneo lingine linalolindwa kama kabati la huduma za nyumbani au gereji. Picha hii inaonyesha mahali ambapo mabomba ya huduma ya maji yanaweza kupatikana katika jengo kwa kawaida.




Bomba la Kawaida la Huduma ya Maji ndani ya Burlington

### *Je, ni nyenzo gani zimeunda mabomba yangu?*

Mabomba ya huduma ya maji ya kipenyo cha inchi 2 na chini yanaweza kuundwa kutoka kwa plastiki, shaba, chuma cha mabati, na risasi. Mabomba ya huduma ya maji ya kipenyo cha zaidi ya inchi 2 yanaweza kuundwa kwa chuma cha kinamo, chuma cha kalibu na plastiki. Tafadhali kagua mwongozo wetu unaoelezea jinsi ya kutambua nyenzo zilizounda mabomba yako ya huduma ya maji.

### *Je, itakuwaje ikiwa nina mabomba mengi ya huduma?*

Ikiwa mali yako ina mabomba mengi ya huduma (kwa mfano, ya matumizi ya nyumbani, ulinzi wa moto na/au umwagiliaji), tafadhali andika kila moja kando. Fomu ya utafiti itakuelekeza kwa utaratibu huo.

### *Siwezi kufikia bomba la maji, nifanye nini?*

Ikiwa unaishi katika jengo lenye nyumba nyingi, tutashirikiana na mmiliki/msimamizi wa mali kutambua bomba la huduma linaloleta maji.

### *Siwezi kufikia sehemu ya chini ya nyumba ili kutambua nyenzo zinazounda bomba langu ya huduma.*


Idara Rasilimali za Maji ya Burlington itakuwa na idadi ndogo ya miadi ya ziara za nyumbani ili kukusaidia kubaini nyenzo za bomba lako la maji. Ikiwa unatarajia kuhitaji ziara ya eneo basi tafadhali wasiliana nasi kwa (802) 863-4501 au tuma barua pepe ili uongezwe kwenye orodha ya wanaosubiri. Idara itawasiliana nawe katika msimu wa Kuchipua wa 2024 kutoa maelezo ya ziada kuhusu jinsi ya kupanga muda wako unaopendelea.

### *Je, itakuwaje ikiwa bomba langu la maji linahitaji kubadilishwa?*

Utaarifiwa ikiwa tumetambua bomba lako la maji kuwa la GRR au la risasi (kuwa uwezekano mdogo) linalohitaji ubadilishaji wakati wa Awamu ya II ya mradi huu. Ikiwa bomba lako la maji linahitaji kubadilishwa, litabadilishwa bila gharama kwako.

### *Kwa matengenezo na ubadilishaji mwingine wa bomba la maji, nina jukumu gani kama mmiliki wa mali?*

Kwa matengenezo na ubadilishaji wa kawaida wa bomba la maji, Jiji la Burlington na mmiliki wa mali hugawana asilimia 50 ya jukumu na gharama kutoka kwa bomba kuu hadi kwenye valvu ya kituo cha kufunga maji. Mmiliki wa mali pia anawajibika kwa asilimia 100 ya gharama za bomba la maji kutoka valvu ya kituo cha kufunga maji hadi nyumbani ikiwa ni pamoja na mita ya maji. Kazi zote za bomba la maji lazima zikamilishwe na Idara ya Rasilimali za Maji ya Burlington isipokuwa kama imeidhinishwa vinginevyo na idara. Picha iliyo hapa chini inaeleza kwa ufupi majukumu ya mmiliki wa mali na Jiji la Burlington kwa kila sehemu ya bomba la huduma ya maji.



## *Je, Jiji la Burlington linachukua hatua gani kuzuia mfiduo wa risasi katika maji yetu ya kunywa?*

Ingawa Jiji la Burlington halina rekodi zozote za mabomba ya huduma ya maji yenye risasi katika Jiji na haitarajii kupata mabomba yoyote ya maji yenye risasi, tunazuia mfiduo wa risasi kwa:

- Kuongeza kizuia kutu kinachoitwa Zinc Orthophosphate kwenye maji. Hii inazuia metali, kama vile risasi na shaba, kuingia ndani ya maji.
- Kutekeleza mpango thabiti wa kupima sampuli ili kufuatilia viwango vya risasi na shaba katika nyumba za makazi ambazo zina uwezekano mkubwa wa kuwa na mfiduo wa risasi kulingana na tarehe yao ya ujenzi.

Aidha, Jimbo la Vermont lilipiga marufuku lehemu za risasi zinazoundwa kwa risasi kwa zaidi ya asilimia 8 mnamo mwaka wa 1988. Katika mwaka wa 2010, Jimbo lilipunguza kiwango cha juu cha risasi kinachoruhusiwa ili kuzingatiwa kuwa "bila risasi" kwa wastani halisi wa asilimia 0.25 kwa vifaa vya mabomba na asilimia 0.20 kwa lehemu au dutu ya kurahisisha kuyeyusha vyuma. Jimbo la Vermont pia lina mojawapo ya mipango madhubuti zaidi ya ufuatiliaji wa risasi nchini kwa shule na vituo vya matunzo ya watoto.

## *Je, ninawezaje kujua ikiwa nina vyanzo vingine vya risasi nyumbani kwangu?*

Mpango wa Risasi wa Burlington ni mpango wa makazi ndani ya Ofisi ya Maendeleo ya Jamii na Uchumi ya Burlington (CEDO). Mpango huu unaweza kutoa elimu, ziara za nyumbani pamoja na uhamasisho na huduma kwa nyumba ndani ya Burlington ili kuzuia mfiduo wa risasi kupitia rangi ya risasi na unaweza kukuunganisha na huduma za ziada, kama vile mpango wa Nyumba zenye Afya (Healthy Homes), ambao unaweza kutoa msaada wa kifedha kushughulikia masuala mengine ya afya na usalama wa mazingira.

Idara ya Afya ya Vermont inaweza kutoa taarifa kuhusu hatari za ziada za risasi ikiwa ni pamoja na zile zinazopatikana kwenye udongo, shughuli za kujiburudisha na ufundi, bidhaa za watumiaji, bidhaa zilizoagizwa kutoka nje na za kale au zilizookolewa.

## *Je, ninawezaje kujikinga kutokana na mfiduo wa risasi katika maji ya kunywa?*

Kwanza, elewa ikiwa unaweza kuwa katika hatari ya kupata risasi nyumbani kwako.

1. **Jifunze kuhusu mfumo wako wa maji ya kunywa.** EPA inahitaji mifumo yote ya maji ya jamii kuandaa na kutoa ripoti ya kila mwaka ya ubora wa maji. Ripoti hii inapatikana kwenye ukurasa wa Ubora wa Maji wa tovuti yetu na inajumuisha matokeo ya sampuli kutoka kwa upimaji katika mfumo wa usambazaji wa Burlington nzima. Nakala za karatasi zinaweza kutumwa kwa barua ukiomba.
2. **Agiza maji yako yapimwe.** Ikiwa una wasiwasi kwamba kunaweza kuwa na risasi katika mabomba nyumbani kwako, kuna huduma inayopatikana ya upimaji. Idara ya Afya ya Vermont hutoa uchambuzi wa kemikali, radiolojia, na mikrobiolojia kwa maji ya kunywa ya umma na ya kibinafsi. Kagua vipimo vinavyopatikana, gharama na maelekezo ya kuchukua sampuli inayofaa kwa kutembelea kiungo kilicho hapo juu au kupiga simu kwa 1-800-660-9997.

Punguza mfiduo wako kwa kuchukua hatua zifuatazo:

1. **Safisha mabomba yako kabla ya kunywa.** Fungulia maji baridi kabla ya kuyatumia kwa dakika 5 wakati wowote ambapo hujatumia maji yako kwa zaidi ya saa 6. Hii huondoa maji kutoka kwa mabomba yako ambayo yanaweza kuwa yamegusa vipengele vya risasi kwa muda mrefu na kuhakikisha kuwa maji yako yanatoka moja kwa moja kutoka kwa bomba kuu.
2. **Tumia vichujio au vifaa vya kutakasa maji.** Zingatia kuweka kichujio cha maji. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu bidhaa hasa zilizoundwa kupunguza risasi kwa kutembelea National Sanitation Foundation.
3. **Badilisha mabomba yako.** Ikiwa unashuku mabomba yako ya ndani yana vipengele vya risasi, tunapendekeza ubadilishe vifaa vya zamani kwa vipya ambavyo vinakidhi masharti ya sasa ya kuzuia mfiduo wa risasi. Unaweza kupata fundi bomba aliyeidhinishwa kufanya kazi katika Vermont kwa kutembelea Idara ya Usalama wa Umma ya Vermont.

Tafadhali kumbuka kuwa Jiji la Burlington tayari limechukua hatua kadhaa kuzuia mfiduo wa risasi katika maji ya kunywa, na kuna uwezekanao mdogo sana wa mfiduo wa risasi.

## *Je, ratiba ya mradi huu ni gani?*

EPA ilitangaza Marekebisho ya Kanuni mnamo mwaka wa 2021 lakini hivi karibuni imetoa mwongozo kwa majimbo kuhusu jinsi ya kutayarisha orodha ya mabomba ya maji. Jiji la Burlington linalenga kupata awamu ya kwanza ya majibu ya wateja kufikia Aprili 2024 ili tuweze kufanya ufuatiliaji na kukamilisha orodha kufikia mwisho wa mwezi wa Oktoba 2024.

## *Nyenzo kwa maswali zaidi kuhusu mfiduo wa risasi*

**Jiji la Burlington**

Mpango wa Risasi wa Burlington: www.burlingtonvt.gov/blp au (802) 865-5323

Ripoti za Ubora wa Maji: www.burlingtonvt.gov/water/Water-Quality-Reports au (802) 863-4501
Timu ya Huduma kwa Wateja: water-resources@burlingtonvt.gov au (802) 863-4501

**Jimbo la Vermont**

Hatari za Risasi Nyumbani: www.healthvermont.gov/environment/home/lead-hazards-and-lead-poisoning
Upimaji wa Maji ya Kunywa: www.healthvermont.gov/lab/drinking-water-testing au 1-800-660-9997
Kanuni na Utekelezaji wa Sheria za Risasi: www.ago.vermont.gov/divisions/consumer-protection/consumer-resources/lead
Mafundi Bomba Walioidhinishwa: www.firesafety.vermont.gov/licensing/plumbing

**Shirika la Ulinzi wa Mazingira la Marekani**

Marekebisho na Kanuni ya Risasi na Shaba: www.epa.gov/dwreginfo/lead-and-copper-rule
Taarifa Zote kuhusu Risasi: www.epa.gov/lead